Habari Leo Jumatano June 24, 2026. Pg 8

# Latra yawaonya wasafirishaji wanaobagua wenye ulemavu

SERIKALI imeiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya watoa huduma za usafiri wa umma wanaowabagua watu wenye ulemavu ikiwemo kufuta leseni kwa watakaobainika kukiuka kanuni zinazolinda haki za kundi hilo.

Maelekezo hayo yalitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalumu, Stella Alex (CCM) aliyekuwa akitaka kufahamu hatua zinazochukuliwa dhidi ya baadhi ya waendeshaji wa usafiri wa umma wanaoendelea kutoza gharama za ziada kwa vifaa saidizi vinavyotumiwa na watu wenye ulemavu.

Akijibu swali hilo, Kihenzile alisema waendeshaji wa usafiri wanaokiuka sheria na kanuni zinazolinda haki za watu wenye ulemavu hawapaswi kuendelea kutoa huduma.

"Iwapo kuna mwendeshaji au mtoa huduma ya usafiri anayewabagua watu wenye ulemavu kwa kutokuzingatia kanuni hizi, hatua stahiki za kisheria zichukuliwe mara moja na pale inapobidi leseni yake ifutwe," alisema.

Alisema serikali imeendelea kuimarisha huduma za usafiri jumuishi kupitia sera, sheria na maendeleo ya miundombinu ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata fursa sawa ya kutumia usafiri wa umma.

Kwa mujibu wa Kihenzile, miradi ya miundombinu ya barabara inaendelea kujumuisha njia za watembea kwa miguu na huduma nyingine za upatikanaji ili kukidhi mahitaji ya watumiaji wote wa barabara, wakiwemo watu wenye ulemavu.

Alisema serikali pia imeweka utaratibu wa kuhakikisha vyombo vya usafiri wa umma vinavyoingizwa nchini vinakuwa na nafasi na vifaa vinavyofaa kwa watumiaji wa viti mwendo na abiria wengine wenye mahitaji maalumu.

"Tunataka watu wenye ulemavu wafurahie haki na fursa sawa na wananchi wengine wote. Upatikanaji wa huduma na kutobaguliwa ni miongoni mwa vipaumbele muhimu katika sekta ya uchukuzi," alisema.

Kihenzile alisema serikali kupitia mamlaka za serikali za mitaa na taasisi nyingine za usimamizi inaendelea kufuatilia utekelezaji wa sera na kanuni zinazolenga kulinda haki na ustawi wa watu wenye ulemavu.

"Watoa huduma wasiokidhi matakwa ya kisheria hawapaswi kupewa leseni za uendeshaji. Huwezi kutoa leseni kwa mwendeshaji anayewabagua watu wenye ulemavu. Sheria iko wazi kuhusu suala hili," alisema.

Kihenzile pia alinukuu Sheria ya Watu Wenye Ulemavu akisema inalenga kukuza usawa, ujumuishaji na ulinzi dhidi ya aina zote za ubaguzi.

Katika swali la msingi, Stella alitaka kujua hatua ambazo serikali imechukua kuhakikisha huduma za usafiri wa umma zinazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu, mbali na usafiri wa ndege na reli ya kisasa (SGR).

Akijibu, Kihenzile alisema Serikali kupitia Kanuni ya 37 ya Kanuni za Leseni za Usafirishaji (magari ya abiria) za mwaka 2020 imeweka sharti kwa watoa huduma kutotoza gharama za ziada kwa vifaa saidizi vinavyotumiwa na watu wenye mahitaji maalumu wanapotumia vyombo vya usafiri.

Aliongeza kuwa Wizara ya Uchukuzi kupitia LATRA kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na wadau wengine imeandaa viwango vya mabasi vinavyohakikisha uwepo wa vifaa maalumu vya kusaidia abiria kupanda na kushuka kwa urahisi, ikiwemo ramps kwa ajili ya watu wenye ulemavu, wazee, watoto na wagonjwa.

CamScanner

**aji wa umeme kitaifa na asilimia 78 vijijini**

HOJA YA HAJA

> **Ni wajibu wa mamlaka husika, viongozi wa stendi, madereva, makondakta na wananchi kwa ujumla kushirikiana kuhakikisha kuwa huduma za usafiri...**

Na HAWA NGADALA

# LATRA imulike mchezo huu mchafu Stendi ya Magufuli

KUMEKUWA na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi wanaotumia usafiri wa mabasi katika Stendi ya Mbezi Mwisho, eneo la Barabara ya Malamba Mawili, Dar es Salaam, kuhusu tabia ya baadhi ya madereva, makondakta na wapiga debe kuwatoza abiria fedha za ziada, zinazodaiwa kuwa ni kuwawekea au kuwahifadhia kiti ndani ya mabasi.

Inadaiwa baadhi ya abiria hulazimika kutoa kati ya sh. 500 na zaidi kupata nafasi ya kukaa kwenye mabasi, huku wanaokataa kutoa fedha hizo wakati mwingine wakikosa kiti au kuachwa nyuma licha ya kufika mapema kituoni.

Jambo hili linaibua maswali kuhusu uhalali wa utaratibu huo, kwani hakuna mamlaka iliyowahi kutangaza rasmi malipo ya kuwekewa kiti katika usafiri wa umma.

Kimsingi, nauli anayolipa abiria ndiyo inayopaswa kugharamia huduma yote ya usafiri, hivyo kutozwa fedha nyingine nje ya utaratibu rasmi kunatafsiriwa kama mzigo usio wa lazima kwa wananchi.

Mbali na kuwaongezea gharama watumiaji wa huduma za usafiri, tabia hiyo inachochea vitendo vya rushwa ndogo vinavyoweza kujengeka na kuonekana kuwa jambo la kawaida katika jamii.

Kiasi hicho cha fedha kinapoendelea kukusanywa kila siku kutoka kwa maelfu ya abiria, huishia kuwa mzigo mkubwa kwa wananchi na manufaa kwa wachache.

Aidha, mfumo huo unaondoa usawa miongoni mwa abiria, badala ya kuzingatia utaratibu wa anayewahi kufika kupata huduma kwanza, nafasi za kukaa hupewa kipaumbele wale wanaotoa fedha za ziada.

Hali hiyo husababisha malalamiko, migogoro na kuvuruga utaratibu unaotakiwa kuwapo katika vituo vya usafiri wa umma.

Kutokana na hali hiyo, mamlaka zinazohusika na usimamizi wa usafiri wa nchi kavu zinapaswa kufanya uchunguzi wa kina kuhusu madai hayo na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wote watakaobainika kukiuka sheria, kanuni na taratibu za utoaji huduma.

Sanjari na hilo, elimu inapaswa kutolewa kwa wananchi ili wafahamu haki zao wanapotumia usafiri wa umma na namna ya kutoa taarifa wanapokutana na vitendo vya aina hiyo.

Uelewa huo utasaidia kudhibiti mianya ya unyonyaji na kuimarisha uwajibikaji kwa wahudumu wa sekta ya usafiri.

Kwa upande wa madereva na makondakta, wanapaswa kutambua kuwa wao ni wahudumu wa umma wenye wajibu wa kutoa huduma kwa haki, usawa na uadilifu kwa abiria wote.

Kushiriki au kufumbia macho utozwaji wa fedha zisizo rasmi kunadhoofisha imani ya wananchi kwa sekta ya usafiri na kuharibu taswira ya taaluma hiyo.

Katika kukomesha tatizo hilo, ukaguzi wa mara kwa mara unapaswa kufanyika katika stendi mbalimbali, hususan Mbezi Mwisho, kubaini na kuwachukulia hatua wanaojihusisha na utozwaji wa fedha kinyume cha utaratibu.

Hatua hizo zitarejesha nidhamu na kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Ni wazi kuwa utozwaji wa fedha kwa madai ya kuwekewa kiti ni jambo linalohitaji kushughulikiwa kwa haraka, endapo hali hiyo itaachwa iendelee, itaongeza mzigo kwa wananchi na kuendeleza mazingira ya unyonyaji yasiyokuwa na tija kwa jamii.

Ni wajibu wa mamlaka husika, viongozi wa stendi, madereva, makondakta na wananchi kwa ujumla kushirikiana kuhakikisha kuwa huduma za usafiri wa umma zinatolewa kwa kuzingatia sheria, haki na usawa.

Usafiri wa umma unapaswa kuwa huduma inayorahisisha maisha ya wananchi, badala ya kuwa chanzo cha kero na gharama zisizo za lazima.

Wakati umefika wa kuchukua hatua madhubuti kurejesha nidhamu, uwazi na uaminifu katika vituo vya usafiri kwa manufaa ya wananchi wote. Hilo ndilo jambo ambalo wananchi wen… wanatarajia kuliona likitekelezwa.

## TULIKOTOKA



RAIS Julius Nyerere, akimsikiliza mwananchi akisoma kitabu, katika darasa la kisomo chenye manufaa (Elimu ya Watu Wazima), mjini Dar es Salaam. Hiyo ilikuwa Mei 15, 1974.